JAMHURI YA MUUNGANO WATANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOGWE

# MUHTASARI WA KIKAO CHA:

## TIMU YA MENEJIMENTI (CMT) YA HALMASHAURI KILICHOFANYIKA KWENYE UKUMBI WA HALMASHAURI TAREHE 18/12/2021

1. **MUHT.NA.MDC/CMT/25/2020/2021/4 - Mahudhurio ya Wajumbe.**

**1.1 Mahudhurio ya Wataalamu:**

| NA | JINA | WADHIFA | NAFASI |
|---|---|---|---|
| 1 | P.K Egidius | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) | Mwenyek |
| 2 | Halima Musuya | Kaimu Afisa Utumishi | Katibu |
| 3 | Lackyp Messay | Kaimu Mwanasheria | Mtaalam |
| 4 | Lawi Misaki | Afisa maendeleo ya jamii | Mtaalam |
| 5 | Kevin R. Charles | Kaimu Mwekahazina | Mtaalam |
| 6 | Dr. Sostenes Nkombe | Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi | Mtaalam |
| 7 | Alen N.Daniel | Kaimu Katibu TSC | Mtaalam |
| 8 | Jastinian Kabulu | Kaimu Afisa Elimu Msingi | Mtaalam |
| 9 | Ahmed S. Abdalah | Kaimu Afisa Elimu Sekondari | Mtaalam |
| 10 | Paul P. Alex | Kaimu Afisa Ugavi na Manunuzi | Mtaalam |

**1.2 Wajumbe Wasiohudhuria Bila Sababu: -Hakuna.**

**1.3 Mahudhurio ya Sekretarieti:**

| NA | JINA | WADHIFA | NAFASI |
|---|---|---|---|
| 1 | Shabani Kimu | Sekretarieti | Mtaalamu |
| 2 | Daud Makoye | Sekretarieti | Mtaalamu |

2. **MUHT. NA. MDC/CMT/25/2020/2021/349 - Kufungua Kikao.**

Mwenyekiti alifungua Kikao Saa 4:18 Asubuhi.

2.1 **MUHT.NA.MDC/CMT/25/2020/2021/5 - Kuridhia Agenda.**

Aidha, baada ya Mwenyekiti kufungua kikao; Wajumbe Kwa pamoja waliridhia agenda za Kikao zifuatazo:

2.1.1 Kufungua Kikao;

2.1.2 Kuridhia Agenda za Kikao;

2.1.3 Maandalizi ya Kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango cha Mwezi Novemba, 2021: -

2.1.3.1 Kupitia taarifa ya Mapato na Matumizi kwa kipindi cha Mwezi Oktoba, 2021;

2.1.3.2 Kupitia Taarifa ya Utawala kwa kipindi cha Mwezi Oktoba, 2021;

2.1.3.3 Taarifa ya Utengenezaji wa gari STK 5175;

2.1.3.4 Taarifa ya uwepo wa Mlipuko wa Machimbo ya dhahabu Kijiji cha Kakumbi Kata ya Lugunga;

2.1.3.5 Taarifa ya kupokea Fedha za Afya na Usafi wa Mazingira (SRWSS) 2020/2021 Tsh. **173,000,000**;

2.1.3.6 Kupitia Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango cha tarehe 22 Novemba, 2021;

2.1.3.7 Kupitia Yatokanayo na kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango cha tarehe 22 Novemba; 2021; Na;

**2.1.4 Kufunga Kikao.**

**3. MUHT.NA.MDC/CMT/25/2020/2021/5 - Maandalizi ya Kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango cha Mwezi Novemba, 2021: -**

3.1 **Kupitia taarifa ya Mapato na Matumizi kwa kipindi cha Mwezi Oktoba, 2021**:

Taarifa ya Mapato na Matumizi katika kipindi cha Mwezi Oktoba 2021 iliwasilishwa na kupokelewa na Wajumbe: Aidha, taarifa Ilifafanua kuwa, kwa Mwaka wa Fedha **2021/2022** Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe imekasimia kukusanya jumla ya Tshs **32,692,230,850/=** kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato.

Vilevile, katika kipindi cha Mwezi Oktoba, 2021 Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe ilikusanya kiasi cha Tshs **242,606,004.00** katika mapato ya ndani, Tshs. **231,340,555.00** katika mapato lindwa na Tshs. **11,265,449.00** na kufanya Jumla ya makusanyo kuwa Tshs. **911,846,897.91** sawa na **57.79%** ya lengo la Mwaka la Tshs. **1,577,800,000.00**.

Aidha, katika makusanyo hayo, vyanzo vya ndani ni Tshs. **853,632,227.00** sawa na **60.56%,** Mapato lindwa ni Tshs. **58,214,670.91** sawa na **34.61%.** Kadhalika, katika kipindi cha Mwezi Oktoba, **2021** Halmashauri imepokea Ruzuku ya Serikali Kuu na Miradi ya Maendeleo yenye jumla ya Tsh **2,020,041,388.00** na kufanya jumla ya Fedha iliyopokelewa Julai-Oktoba,2021 kuwa Tshs. **6,672,626,123.00** sawa na **21.44%** ya lengo la Mwaka la Tshs. **31,114,430,850** ambapo mapato ya ruzuku ni Tshs. **306,003,886.00**, Mishahara Tshs. **5,294,099,550.00** na fedha za Maendeleo Tsh. **1,072,522,687.00.**

Pia, Katika kipindi cha Mwezi Oktoba, **2021** kiasi cha Tshs. **118,350,000** kimepokelewa kama nguvu za Wananchi zilizothaminiwa na kufanya jumla ya mapato ya Mwezi Julai- Oktoba, 2021 kuwa Tshs. **6,790,976,123.00** sawa na **21.82%** ya lengo la Mwaka **2021/2022**.

Vilevile, katika kipindi cha Mwezi Oktoba, 2021 Halmashauri imepokea Fedha za UVIKO-19 kiasi cha Tshs. **80,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa

Bweni la Wanafunzi Maalum Shule ya Msingi Masumbwe, Tshs. **1,580,000,000.00** kwa ajili ujenzi wa Madarasa Shule za Sekondari, Tshs **120,000,000.00** kwa ajili ya Ujenzi wa Madarasa Shule Shikizi–Msingi na kufanya Jumla ya Fedha za UVIKO -19 zilizopokelewa Mashuleni kuwa Tshs. **1,870,000,000.00.**

| TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA IMF | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Na** | **Jina la Mkoa** | **Jina la Halmashuri** | **Jina la Kituo** | **Aina ya mradi** | **Tarehe ya kupokea fedha** | **Kiasi cha Fedha kilichopokelewa Tsh** | **Chanzo cha Fedha** |
| 1 | Geita | Mbogwe | Shule ya Secondari ISANGIJO | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 3 katika Shule ya Secondari ISANGIJO | 15/10/2021 | 60,000,000 | UVIKO - 19 |
| 2 | Geita | Mbogwe | Shule ya Secondari NYASATO | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 8 katika Shule ya Secondari NYASATO | 15/10/2021 | 160,000,000 | UVIKO - 19 |
| 3 | Geita | Mbogwe | Shule ya Secondari MASUMBWE | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 11 katika Shule ya Secondari MASUMBWE | 15/10/2021 | 220,000,000 | UVIKO - 19 |
| 4 | Geita | Mbogwe | Shule ya Secondari NHOMOLWA | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 3 katika Shule ya Secondari NHOMOLWA | 15/10/2021 | 60,000,000 | UVIKO - 19 |
| 5 | Geita | Mbogwe | Shule ya Secondari NGEMO | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 4 katika Shule ya Secondari NGEMO | 15/10/2021 | 80,000,000 | UVIKO - 19 |
| 6 | Geita | Mbogwe | Shule ya Secondari NANDA | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 3 katika Shule ya Secondari NANDA | 15/10/2021 | 60,000,000 | UVIKO - 19 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 7 | Geita | Mbogwe | Shule ya Secondari MBOGWE | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 4 katika Shule ya Secondari MBOGWE | 15/10/2021 | 80,000,000 | UVIKO - 19 |
| 8 | Geita | Mbogwe | Shule ya Secondari MBOGWE | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 9 katika Shule ya Secondari MBOGWE | 15/10/2021 | 180,000,000 | UVIKO - 19 |
| 9 | Geita | Mbogwe | Shule ya Secondari LULEMBELA | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 6 katika Shule ya Secondari LULEMBELA | 15/10/2021 | 120,000,000 | UVIKO - 19 |
| 10 | Geita | Mbogwe | Shule ya Secondari LUGUNGA | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 6 katika Shule ya Secondari LUGUNGA | 15/10/2021 | 120,000,000 | UVIKO - 19 |
| 11 | Geita | Mbogwe | Shule ya Secondari ISEBYA | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 6 katika Shule ya Secondari ISEBYA | 15/10/2021 | 120,000,000 | UVIKO - 19 |
| 12 | Geita | Mbogwe | Shule ya Secondari IPONYA | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 3 katika Shule ya Secondari IPONYA | 15/10/2021 | 60,000,000 | UVIKO - 19 |
| 13 | Geita | Mbogwe | Shule ya Secondari ILOLANGULU | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 4 katika Shule ya Secondari ILOLANGULU | 15/10/2021 | 80,000,000 | UVIKO - 19 |
| 14 | Geita | Mbogwe | Shule ya Secondari IKUNGUIGAZI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 3 katika Shule ya Secondari IKUNGUIGAZI | 15/10/2021 | 60,000,000 | UVIKO - 19 |
| 15 | Geita | Mbogwe | Shule ya Secondari IKOBE | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 3 katika Shule ya Secondari IKOBE | 15/10/2021 | 60,000,000 | UVIKO - 19 |
| 16 | Geita | Mbogwe | Shule ya Secondari | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 3 katika Shule ya Secondari | 15/10/2021 | 60,000,000 | UVIKO - 19 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | KANEGERE | KANEGERE | | | |
| 17 | Geita | Mbogwe | Shule ya Msingi ILYAMCHELE | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 katika Shule ya Msingi ILYAMCHELE | 23/11/2021 | 40,000,000 | UVIKO - 19 |
| 18 | Geita | Mbogwe | Shule ya Msing KAGONGO | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 katika Shule ya Msing KAGONGO | 15/10/2021 | 40,000,000 | UVIKO - 19 |
| 19 | Geita | Mbogwe | Shule ya Msing KADOKE | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 katika Shule ya Msing KADOKE | 15/10/2021 | 40,000,000 | UVIKO - 19 |
| 20 | Geita | Mbogwe | Shule ya Msingi MASUMBWE | Ujenzi wa bweni la watoto wenye mahitaji maalum katika Shule ya Msingi MASUMBWE | 15/10/2021 | 80,000,000 | UVIKO - 19 |
| 21 | Geita | Mbogwe | Kituo cha Afya Kagera | Ujenzi wa nyumba ya watumishi wa Afya katika Kituo cha Afya Kagera | 18/02/2022 | 90,000,000 | UVIKO - 19 |
| **JUMLA KUU** | | | | | | **1,870,000,000** | |

**Kwa upande wa Matumizi**, katika kipindi cha Mwezi Oktoba, 2021, Halmashauri imetumia kiasi cha Tshs. **200,666, 479.91** kutoka katika makusanyo yake ya ndani na kufanya ya Matumizi Julai- Oktoba, 2021 kuwa Tshs. **437,321,240.91** sawa na **27.71%** ya lengo la Mwaka. **Aidha**, kiasi cha Tshs **97,042,401.60** kimetengwa katika Akaunti ya Maendeleo kama **40%** ya Miradi ya Miradi ya Maendeleo.

Pamoja na hayo, kwa kipindi cha Mwezi Oktoba, 2021 Halmashauri imetumia Kiasi cha Tshs **1,751,101,510.00** katika fedha za Ruzuku na Miradi ya Maendeleo na kufanya jumla ya matumizi ya Julai- Oktoba, 2021 kuwa Tshs. **6,151,954,383.00** sawa na **19.77%** ya lengo la Mwaka.

Aidha, katika kipindi hicho thamani ya matumizi ya nguvu za Wananchi ilikuwa Tshs. **118,350,000.00** na kufanya jumla ya Matumizi yote ya Halmashauri kuwa Tshs. **6,270,304,383.00** sawa **19.17%** ya lengo la Mwaka.

Pia, taarifa iliendelea kufafanua kuwa, katika kipindi cha kuishia tarehe 31 Oktoba, 2021 Halmashauri ilikuwa na Salio la fedha kama **ifuatavyo:** Salio anzia la Mapato ya ndani Tshs. **230,689,180.20**, Fedha lindwa Tshs.**0.00**, Mapato mengineyo Tshs. **61,785,896.00**, Mishahara Tshs.**0.00**, Fedha za MaendeleoTshs. **1,401,414,799.00** na kufanya jumla ya Tshs. **1,693,889,875.20**.

Kadhalika, katika makusanyo kulikuwa na Salio la katika Mapato ya ndani la Tshs **242,606,004.00**, Tshs **11,265,449.00** kwenye fedha lindwa, Tshs. **40,535,834.00** katika Mapato mengineyo, Tshs **1,317,847,450** kwenye fedha za Mishahara na Tshs **661,658,104** za Maendeleo na kufanya jumla ya Tshs **2,273,912,841**.

Katika Matumizi na Uhamisho 40% kulikuwa na salio la Mapato ya ndani kiasi cha Tshs **271,443,431.60**, Tshs **11,265,449.00** katika fedha lindwa, Tshs **38,205,000.00** katika mapato mengineyo, Tshs. **1,317,847,450.00** za

Mishahara na Tshs **395,049,060.00** zikiwa ni fedha za Maendeleo na kufanya jumla ya Tshs. **2,033,810,390.60**.

Katika Bakaa, kulikuwa na salio la mapato ya ndani kiasi cha Tsh. **201,851,752.60**, Tshs.**0.00** katika fedha lindwa, Tshs. **64,116,730.00 za** Mapato mengineyo, Mishahara Tshs **0.00**, na fedha za Maendeleo Tshs. **1,668,023,843** na kufanya jumla ya Tshs **1,933,992,325.60.**

**Wajumbe kwa pamoja waliridhia makusanyo yaliyofanyika. Taarifa ilipitishwa.**

3.2**Kupitia Taarifa ya Utawala kwa kipindi cha Mwezi Oktoba, 2021: -** Taarifa iliyowasilishwa na kupokelewa na Wajumbe ilihusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali yanayohusu masuala ya kiutumishi ikiwa ni pamoja na kuendelea kuhudumia Watumishi kwa kuzingatia sheria kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali ya utumishi wa umma, usimamizi wa nidhamu, utendaji kazi pamoja na kushughulikia taarifa mbalimbali za kiutumishi na maslahi yao.
Taarifa iliendelea kufafanua kuwa, katika kipindi cha Mwezi Oktoba, **2021** kulikuwa na jumla ya Watumishi **1678,** Mtumishi **1** alihama na **1** alihamia katika Wilaya ya Mbogwe. Kadhalika, katika kipindi hicho Halmashauri ilitembelewa na Wageni **25,** Wageni **15** walitoka nje ya Mkoa, 8 walitoka ndani ya Mkoa na **2** walitoka ndani ya Wilaya.

Aidha, taarifa ilieleza kuwa, Watumishi **2** waliondolewa kwenye mfumo wa malipo ya Mishahara baada ya kukoma utumishi wao kwa sababu ya kufukuzwa kazi pamoja na taarifa hiyo kuonesha madeni mbalimbali

yaliyolipwa kwa Watumishi **9** ikiwa ni fedha za kujikimu zenye Jumla ya Tshs. **3,276,000**.

Kadhalika, taarifa ilibainisha changamoto mbalimbali za Idara ya Utawala na rasilimali watu za upungufu wa magari katika Halmashauri inayosababisha Idara kushindwa kufanya usimamizi wa karibu kwa Watumishi ndani ya Wilaya. **Taarifa ilipitishwa.**

3.3 **MUHT.NA.MDC/CMT/25/2020/2021/5 -Taarifa ya Utengenezaji wa gari STK 5175** Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa na Wajumbe. Ilihusu **profoma invoce** na hatima ya matengenezo ya gari aina ya STK **5175** ambalo lilipata ajali na kupelekwa TEMESA kama taratibu zinavyoelekeza na baadaye TEMESA kuagiza gari hilo kupelekwa FORTES ambapo awali kampuni hiyo ilitoa PROFAMA INVOCE kwa mchanganuo wa gharama halisi za matengezo kuwa Tshs **30,229,122.00**, TRA na VAT 18% Tsh. **5,441,241.96** na kufanya Jumla ya Tsh **35,670,363.96.**

Aidha, taarifa iliendelea kufafanua kuwa, baada ya Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango kupewa gharama hizo na kuabaini kuwa ni kubwa; Kamati iliagiza Menejimenti kufanya mawasiliano na kampuni ya **FORTES** ili iweze kupunguza gharama za matengezo ya gari hilo.

Menejimenti iliwasiliana na Kampuni **FORTES** kama ilivyoagizwa na Kamati ambapo katika Mwezi Novemba 2021 kampuni husika ilikubali kufanya usuluhishi wa gharama za Matengenezo ya gari hilo na kuwa ifuatavyo: - gharama halisi za matengenezo kiasi cha Tshs. **22,857,733.40**,

gharama za TRA (**VAT 18%**) kiasi cha Tshs. **4,114,392.01** na ambapo jumla yake ni kiasi cha Tshs **26,972,125.41**.

Wajumbe walipitisha taarifa hiyo kwa ajili ya kuwasilishwa kwenye Kikao cha kamati ya Fedha, Utawala na Mipango.

**3.4 MUHT.NA.MDC/CMT/25/2020/2021-Taarifa ya uwepo wa Mlipuko wa Machimbo ya dhahabu Kijiji cha Kakumbi Kata ya Lugunga**:

Taarifa iliyowasilishwa na kupokelewa na Wajumbe iliyohusu uwepo wa mlipuko wa machimbo ya dhahabu kwa wachimbaji wadogo wadogo ambapo eneo lenye machimbo lipo chini ya PML (primary Mining Lencese) ambao kwayo ndiye wasimamizi wa mgodi huo.

Aidha, taarifa iliendelea kufafanua kuwa shughuli za uchimbaji madini zinaendelea katika eneo hilo lililopo kwenye Ofisi ya Kijiji cha Kakumbi na maeneo jirani na kuongeza kuwa, mgawo wa kwanza unatokana na machimbo hayo utafanyika tarehe **10/12/2021.** Pia, ilielezwa kuwa, Menejimenti imejipanga kukusanya kikamilifu mapato yanayotokana na machimbo hayo.

Kadhalika, taarifa ilifafanua mapendekezo yaliyotolewa na Menejimenti yafuatayo: - Ushuru wote unaohusu Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) kwa mujibu wa sheria uendelee kusimamiwa na kutozwa ipasavyo, kila Mfuko wa Mchanga/Mawe unaotoka ardhini bila kujali anayemiliki mfuko huo utozwe Ushuru wa Tshs.**1000** ambapo pia itahusisha Migodi yote iliyopo katika Wilaya ya Mbogwe.

Aidha, mapendekezo ya Menejimenti yaliendelea kueleza kuwa, Mwenye Leseni ya Utafiti katika eneo hilo ajenge Ofisi nyingine yenye ramani inayofanana na Ofisi ya Kijiji cha Kakumbi ambayo imeathirika na machimbo hayo pamoja na kuongeza kuwa Mgawo unaotambulika kuwa wa mwenye shamba katika eneo husika ugawanywe nusu kwa Serikali ya Kijiji na Halmashauri ya Wilaya. **Taarifa ilipitishwa.**

**3.5 Taarifa ya kupokea Fedha za Afya na Usafi wa Mazingira (SRWSS) 2020/2021 Tsh. 173,000,000:**

Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa na Wajumbe. Ilihusu mapokezi ya fedha Tshs. **173,000,000** zilizoingia mwishoni mwa Mwezi Novemba 2021 kwa ajili ya uboreshaji miundombinu ya maji na usafi wa mazingira kwenye Vituo vya kutolea huduma za Afya. Aidha, mapokezi hayo ni ya awamu ya pili katika vituo 5 vilivyosalia baada ya Halmashauri kupokea fedha za Ujenzi wa Vituo 12 katika awamu ya kwanza.

Pia, taarifa ilifafanua kuwa, vituo vilivyopokea fedha hizo za awamu ya pili ni Mlange kiasi cha Tshs **32,532,300**, Bwelwa Tshs **28,600,000**, Iponya Tshs **23,000,000**, Nyanghwiga **35,000,000** na Ilangale Tshs. **32,532,300** na kufanya jumla ya Tshs. **151,664,600** ya fedha zilizopokelewa na vituo husika vimepokea fedha hizo katika Akaunti za vituo.

Kadhalika, katika mapokezi ya fedha hizo; fedha za Zahanati ya Iponya zimetumwa na kupokelewa kimakosa ambapo zimetumwa kwenda Zahanati ya Ilolangulu na taratibu za kuzirejesha fedha husika zimefanyika kwa Wizara ya Afya kuandikiwa barua ili iweze kuzirudisha.

Hata hivyo, fedha kiasi cha Tshs. **21,335,400** zitatumika kwa ajili ya usimamizi na uratibu ujenzi wa vyoo ngazi ya Kaya. **Taarifa ilipitishwa.**

**3.6 Kupitia Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango cha tarehe 22 Novemba, 2021**:

Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango cha tarehe 22 Novemba, 2021 ulipitiwa na wajumbe na kufanyiwa masahihisho kadhaa kisha kupitishwa.

**3.7 Kupitia Yatokanayo na kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango cha tarehe 22 Novemba; 2021:**

Taarifa ya yatokanayo iliwasilishwa na kupokelewa na Wajumbe ikiwa na maagizo ya Baraza la madiwani la tarehe 01/12/2021 yaliyokasimiwa kwenye Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango.

Aidha, Wajumbe walikubaliana na utekelezaji wa maagizo hayo ambayo kwayo yatawasilishwa kwenye kikao cha FUM. **Taarifa ilipitishwa**.

4.**MUHT.NA.MDC/CMT/25/2020/2021/5- Kufunga Kikao**.

Mheshimiwa Mwenyekiti alifunga Kikao saa **11.51** Asubuhi.

**'UMETHIBITISHWA NA;**

| | |
|---|---|
| Saini.............................. | Saini ............................ |
| Jina. P.K Egidius | Jina. Halima Musuya |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |
| 18/12/ 2021 | 18/12/2021 |